



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA NISHATI
SHIRIKA LA MAENDELEO YA PETROLI
TANZANIA (TPDC)



TAARIFA KWA UMMA

TATHMINI YA AWALI YA ATHARI ZA KIMAZINGIRA NA KIJAMII JUU YA MRADI WA UTAFITI WA MAFUTA NA GESI ASILIA UNAOTARAJIWA KUFANYIKA KWA NJIA YA MITETEMO (2D SEISMIC DATA ACQUISITION), KATIKA KITALU CHA EYASI WEMBERE KINACHOGUSA MIKOA YA TABORA (IGUNGA), SHINYANGA (KISHAPU), SINGIDA (IRAMBA) NA SIMIYU (MEATU)

TPDC inapanga kufanya utafiti wa mafuta na gesi asilia katika kitalu cha Eyasi wembere kwa kutumia njia ya mitetemo ili kuweza kubaini kwa ufasaha uwezekano wa uwepo wa rasilimali hiyo katika eneo hilo. Kitalu cha Eyasi- Wembere kipo kaskazini mwa Tanzania pembezoni mwa bonde la ufa la Afrika Mashariki. Kitalu kina ukubwa wa takribani Kilomita za mraba 10,640 na kinajumuisha mabonde ya Eyasi, Wembere na Manonga.

Ili kutimiza matakwa ya sheria ya mazingira Sura ya 191 (Namba 20) ya 2004 pamoja na kanuni za tathmini na ukaguzi wa mazingira za mwaka 2005 na mabadiliko yake ya mwaka 2018, taarifa hii inatolewa kwa lengo la kuutaarifu umma kwamba, kampuni ya MTL Consulting Limited kwa kushirikiana na kampuni ya Energy Intel Limited, wamepewa kazi ya kufanya tathmini za awali za athari za kimazingira na kijamii kwa niaba ya Shirika la Maendeleo ya Petroli (Tanzania Petroleum Development Corporation - TPDC) kwa ajili ya mradi wa utafiti wa mafuta na gesi asilia, katika kitalu cha Eyasi wembere kwa kutumia njia ya mitetemo. Tathmini za athari za mazingira na masuala ya kijamii zitajumuisha Mikoa mine (4) inayopitiwa na kitalu hicho ambayo ni Tabora (Igunga), Shinyanga (Kishapu), Singida (Iramba) na Simiyu (Meatu).

Aidha, taarifa hii inatolewa kwa madhumuni ya kutafuta maoni ya pande zote zinazohusika na zitakazoathirika na uwepo wa mradi huu. Mtu yeyote mwenye nia, maoni ama dukuduku au ufahamu kuhusiana na athari za mazingira na kijamii zinazoweza kutokea kutokana na uwepo wa mradi huu anaweza kuwasiliana au kuwasilisha maoni yake kwa maandishi kwa anuani zifuatazo:

Managing Director,
Tanzania Petroleum Development Corporation (TPDC),
Benjamin William Mkapa Towers,
Tower "A", Azikiwe / Jamhuri Street
10th Floor, Room No1011
P.O Box 2774
Dar es Salaam, Tanzania
Tel: +255 22 2200 103/4
Email: info@tpdc.co.tz

The Director General,
National Environmental Management Council (NEMC),
P.O. Box 63154, Regent Estate,
Dar es Salaam, Tanzania.
Tel: +255 22 2774889
Email: nemc@nemctz.org

MTL Consulting Company Limited
Masaki, Plot No. 689
Sandvik Street
P.O. Box 77894
Dar es Salaam.
Tel: +255 22 2600594,
Mobile: +255 754882466
Email: info@mtlconsulting-tz.com